JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni, 2023

Dodoma



Edit with WPS Office

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za Simu…………………..

Mkuu wa Shule… 0754747643

Makamu Mkuu wa Shule. 0752250266

Matron/Patron. 0742987202

Shule ya Sekondari GANAKO

S.L.P.180, KARATU.

Tarehe ….13/06/2023

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….
……………………………………………..
S.L.P ……………………………………..
…………………………………………….

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI GANAKO HALMASHAURI YA KARATU MKOA ARUSHA MWAKA ……2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka…2023/2024 na atasoma tahasusi ya ……..……



Edit with WPS Office

Shule ya Sekondari GANAKO ipo umbali wa Kilometa 1.5 Kaskazini mwa Mji wa …KARATU. Usafiri wa basi kutoka mjini ………… unapatikana katika kituo cha mabasi ……… Nauli ni Shilingi 1500 kwa pikipiki na Shilingi 3000 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 3/7/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/8/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/8/2023.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

| S/N | AINA YA NGUO | IDADI | RANGI |
|---|---|---|---|
| 1 | SURUALI ZA DARASANI ZENYE RINDA(CELABRATION 2) | 2 | BLUU (DARK BLUE) IWE NA TURN UP |
| | SHATI | 2 | NYEUPE(mikono mirefu) |
| | SWETA YENYE V- SHINGONI | 2 | BLUU (DARK BLUE) |
| | KOTI YENYE VIFUNGO VITATU ISIWE NA MPASUO NYUMA | 1 | BLUU (DARK BLUE |
| | SURUALI YA KUSHINDIA | 2 | RANGI YA UGORO |
| | T-SHIRT YENYE COLA (BLUU) | 2 | INAPATIKANA SHULENI KWA TSH 15000/= |
| | VIATU VENYE KISIGINO FUPI NA GIDAMU | JOZI 2 | NYEUSI |
| | SOCKSI | JOZI 2 | RANGI YA BLUU |
| | RABA YA MICHEZO | 1 | |
| | BUCTA YA MICHEZO | 2 | |
| | TRUCKSUIT ISIYO YA MODO | 1 | BLUU(DARK BLUE) |
| | TAI NDEFU | 2 | BLUU(DARK BLUE) |
| | MKANDA WA NGOZI WA KUVALIA SURUALI | 1 | MWEUSI |
| | | | |

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

1. RIMU A4 2.(AINA YA NO1) KWA MWAKA
2. MADAFTARI YA COUNTER Q 3 na Q4 YA KUTOSHA
3. AJE NA GODORO FUTI 2.5 KWA 6
4. BLANKETI 1, MTO NA NETI YA MBU RANGI YA BLUU(aje navyo)



Edit with WPS Office

5. SHUKA MBILI RANGI YA BLUE COTTON (Aje navyo)
6. SAHANI, KIJIKO, BAKULI NA KIKOMBE CHA BATI (Aje navyo)
7. SANDUKU LA BATI LA KUHIFADHIA VIFAA VYAKE (Aje nayo)
8. VITABU VYA MASOMO NUNUA KULINGANA NA TAHASUSI HUSIKA,(KAMUSI/DICTIONARY)
9. NDOO 2 ZA LITA 10 KWA MATUMIZI YAKE ZENYE MIFUNIKO
10. (HGL ) WAJE NA HARD BROOM (1), RUBERSQUIZER (1) NA FAGIO (CHELEWA)
11. ( HGK ) WAJE NA HARD BROOM(1) RUBERSQUIZER (1) NA FAGIO (CHELEWA
12. MATHEMATICAL SET AJE NAYO
13. JEMBE (1) LENYE MPINI
14. CHETI CHA KUZALIWA AJE NACHO
15. RESULTS SLIP ORIGINAL AJE NAYO

### 2.3 Michango mbalimbali

#### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

- **Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule A/C Na. 40910005625 NMB Jina la akaunti Ganako Sec School Development. Mwanafunzi aje na stakabadhi ya malipo ya benki iliyoandikwa jina lake kwa usahihi.**

**NB. KILA MWANAFUNZI AJE NA BIMA YA AFYA KWA AJILI YA MATIBABU.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na



Edit with WPS Office

Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**



Edit with WPS Office

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi




Edit with WPS Office

wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII




**Jina la Mkuu wa Shule SULLEY M H**

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule …… 0754747643
- Makamu Mkuu wa Shule … 0752250266
- Mwandamizi Taaluma … 0762333769
- Mwandamizi Malezi … 0745987202



Edit with WPS Office

KUMB.NA.GSS/K.5/VOL.3/05

FOMU YA HALI YA AFYA YA MWANAFUNZI.

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………………………..

Daktari wa hospitali ya serikali athibitishe kuwepo au kutokuwepo kwa magonjwa yafuatayo kwa mwanafunzi;

1. Kifua kikuu ………………………………………………………………..
2. Ugonjwa wa figo…………………………………………………………………
3. Ugonjwa wa moyo……………………………………………………………
4. Ugonjwa wa akili…………………………………………………………………
5. Ugonjwa wa kisukari…………………………………………………………
6. Ugonjwa wa zinaa…………………………………………………………………
7. Vidonda vya tumbo …………………………………………………………………
8. Ulemavu wowote……………………………………………………………………………
9. Kifafa ……………………………………………………………………………………………
10. Ajali kubwa……………………………………………………………………………………………
11. Tatizo lingine la kiafya…………………………………………………………………………

KWA MATUMIZI YA OFISI TU:

Kwa Daktari anayehusika;

Tafadhali mpime mwanafunzi tajwa hapo juu ili kubaini kama afya yake inaruhusu kuendelea na masomo yake ya kidato cha TANO au la.

MAELEZO YA DAKTARI:



Edit with WPS Office

……………………..........................................................................................................................

Jina la Daktari……………………………………………………………..,

Sahihi…………………………………………..

Muhuri wa Daktari……………………………………………………… Tarehe…

A: HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ------------------------------------------------------------------------------------------- (majina matatu.)

2. Tarehe ya kuzaliwa --------------------------------------------------- (kama ilivyo kwenye cheti cha kuzaliwa )

3. Dini ------------------------------------------------------------------ Dhehebu -----------------------------------------------------

4. Mahali na wilaya alipozaliwa -----------------------------------------------------------------------------------------------

5. Shule ya sekondari alimohitimu (kidato cha nne)/kiwango kingine cha elimu alichofikia na mwaka

----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------- --------

6. Kazi anayofanya ------------------------------------------------------------------------------------------------------------

7. Mambo anayopenda kufanya nje ya masomo-----------------------------------------------------------------------

B: HABARI ZA MZAZI /MLEZI

1. Jina kamili la Baba ------------------------------------------------------------------ ( majina matatu )

2. Kazi yake -------------------------------------------------- Dini -----------------------------------------------------

3. Jina kamili la mama -------------------------------------------------------------------( majina matatu )

4. Kazi yake ----------------------------------------------- Dini ----------------------------------------------

5. Anwani ya mzazi /mlezi -------------------------------------------------------------------------------

6. Namba ya simu ya baba /mama/ mlezi -----------------------------------------------------------------

7. Kijiji/mtaa anamoishi --------------------------------- Kata ---------------------- Wilaya---------

8. Jina la balozi au M/kiti wa mtaa.--------------------------------------- namba ya simu---------------------

9. Sahihi na Muhuri wa M/kiti wa mtaa anamoishi.------------------------------------------------------------------

picha



Edit with WPS Office

UTHIBITISHO WA MZAZI /MLEZI

“Ninaahidi kuwa nitashirikiana na walimu kusimamia nidhamu ya mwanangu ,nitatii wito wowote nitakapo

hitajika shuleni na nitahakikisha kuwa mwanangu atatii sheria na kanuni zote za shule hii”.

JINA LA MZAZI /MLEZI--------------------------------------------------- SAHIHI---------------------------------------------

TAREHE-----------------------------------------



Edit with WPS Office